TANGAZO LA SERIKALI Na. 275 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 (1) na 16(1))*

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI, 2021

Jina na tarehe ya kuanza Sheria kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli ya mwaka 2021.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakavyoelekezwa vinginevyo;

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli.

"gari" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine na chenye leseni ya kufanya shughuli hiyo.

"kibali cha ujenzi" maana yake ni kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi ambao unafanyika ndani ya eneo la Mamlaka ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii au Kanuni na Sheria zinazosimamia ujenzi.

"maegesho" maana yake ni sehemu au eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha magari au vyombo vya usafiri au vyombo vya moto.

"mazao" maana yake ni mazao yote yatokanayo na shughuli za mashambani ikijumuisha mazao ya Chakula, biashara pamoja na mazao ya misitu.

"matangazo" maana yake ni matangazo yanayotangazwa kwa kutumia vipaza sauti kwa ajili ya kutangaza biashara ya aina yeyote katika eneo la Halmashauri ikijumuisha matangazo katika masoko, magulio, sherehe, mikutano isipokuwa matangazo ya vifo au misiba.

Sura ya 323

"mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 2 cha Sheria ya Misitu.

"minara" maana yake ni minara yote itakayowekwa kwa ajili ya mawasiliano ya simu, fax, redio yenye urefu unaozidi mita ishirini (20) kutoka usawa wa ardhi.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi kwa wakati huo.

"Chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu, mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine na

chenye leseni ya kufanya shughuli hiyo ambavyo ni teksi, malori, mabasi, magari binafsi, pikipiki, bajaji, kirikuu na vingine vinavyofanana na hivyo isipokuwa baiskeli au guta.

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa Soko" maana yake ni ushuru ambao hutozwa kutokanana na bidhaa zinazoletwa na kuuzwa katika masoko na magulio yanayomilikiwa na Halmashauri.

"vizimba" maana yake ni vibanda vidogo vidogo vilivyojengwa ndani ya eneo la soko au vibanda vinavyohamishika ambavyo vimewekwa ndani ya eneo la soko kwa mfano vibanda vya makampuni ya simu, na vingine vinavyouza bidhaa mbalimbali.

"Wakala" maana yake ni mtu, Shirika, Kampuni, Taasisi au Asasi yoyote iliyoingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru kwa niaba yake.

Ada na Ushuru

3(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada na Ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hii utatakiwa kulipwa kabla au wakati wa huduma kutolewa.

(3) Ada na Ushuru utakaotozwa utalipwa kwa Halmashauri au Wakala ambaye ameteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya Ada na Ushuru husika kwa niaba yake.

(4) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kwa stakabadhi ya kielektroniki.

## SURA YA PILI
## ADA YA UPIMAJI AFYA

Upimaji Afya

4(1) Litakuwa ni jukumu chini ya Sheria Ndogo hii kwa kila mhudumu wa baa, hoteli, mgahawa, mama lishe na baba lishe, nyumba za kulala wageni na wahudumu wote wa vyakula na vinywaji wanaohudumia jamii kibiashara pamoja na wafanyakazi wa viwandani kupima afya zao kila baada ya miezi sita na kulipa ada za Upimaji afya kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote atakayetoa huduma bila kupima afya yake atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kulipa faini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii pamoja na kusitishwa kutoa huduma husika mpaka pale atakapopima afya yake.

## SURA YA TATU
## ADA YA VIBALI VYA UJENZI

Vibali vya Ujenzi

5(1) Ni wajibu wa kila mtu, taasisi, kikundi, Kampuni yoyote chini ya Sheria Ndogo hii pamoja na Sheria na Kanuni zinazosimamia ujenzi mijini kabla ya kuanza ujenzi wa aina yoyote ile kuomba kibali cha ujenzi kwa Halmashauri na kulipa ada kabla ya kuanza ujenzi husika.

(2) Halmashauri itatoza ada kwa ajili ya vibali vya ujenzi kwa viwango vinavyoonyeshwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii kulingana na ukubwa wa eneo.

(3) Maombi ya kibali cha ujenzi yatawasilishwa pamoja na ramani ya ujenzi.

(4) Mtu, taasisi, kikundi au kampuni yoyote

itakayoanza ujenzi bila kupata kibali cha ujenzi, itakuwa imetenda kosa na atatakiwa kusimamisha ujenzi mpaka itakapopata kibali husika.

## SURA YA NNE
## ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

Ada ya Ukaguzi wa Nyama

6(1) Kila mnyama atakayechinjwa kwenye machinjio au eneo lingine lililoruhusiwa ndani ya Halmashauri atapaswa kulipiwa ada ya ukaguzi wa nyama kwa kiwango kama kilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza, kugawa au kusambaza nyama kwa ajili ya matumizi ya watu kabla ya kukaguliwa kama inafaa kwa matumizi ya binadamu.

## SURA YA TANO
## USHURU WA SOKO LA WANYAMA

Ushuru wa Soko la Wanyama

7. Halmashauri itatoza ushuru wa soko kwa kila mnyama atakayeuzwa au kununuliwa katika soko la wanyama kwa viwango kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii.

## SURA YA SITA
## KODI, USHURU NA ADA KWA MATUMIZI YA MASOKO NA MAGULIO

Tozo kodi, ushuru na ada

8(1) Halmashauri itatoza;

(a) kodi ya pango kwa chumba au fremu au kibanda kwa majengo ya biashara yanamilikiwa na Halmashauri,

(b) ushuru wa masoko pamoja na ada mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya masoko na magulio kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Sita la Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kubadilisha kodi pale ambapo itaona inafaa na mabadiliko ya

kodi husika yatakuwa halali kutozwa baada ya kurekebisha Sheria Ndogo husika.

SURA YA SABA
USHURU WA MAZAO YA BIASHARA NA MISITU

Halmashauri kutoza Ushuru wa Mazao.

9 (1) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao kwa mazao yote ya biashara, chakula na misitu yatakayozalishwa ndani ya eneo la Halmashauri pamoja na mazao yote yatakayoingizwa ndani ya eneo la Halmashauri kutoka eneo linguine kama ikithibitika kuwa hayajatozwa ushuru wa mazao huko yatokako.

(2) Ushuru wa mazao utatozwa kutoka kwa kila mnunuzi kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Saba la Sheria Ndogo hii ya bei ya kununulia zao husika.

(3) Mnunuzi au mtu mwingine yeyote atakayesafirisha mazao yake nje ya eneo la Halmashauri atawajibika kulipa ushuru.

(4) Kila mnunuzi wa mazao atatakiwa kujisajili kwa ajili ya kununua mazao ndani ya Halmashauri, na baada ya usajili atapewa kibali cha maandishi cha kununua mazao hayo.

(5) Kibali kitakachotolewa chini ya kifungu cha 9(4) kitaonyesha:

a) jina la zao husika,
b) kiasi cha mazao,
c) kiasi cha ushuru utakaotozwa kwa ajili ya mazao yanayoombewa kibali,
d) eneo ambapo mazao hayo yatanunuliwa.

(6) Halmashauri inaweza kukataa kutoa kibali kwa mnunuzi yeyote ambaye anadaiwa ushuru wa mazao au kwa kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hii.

(7) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi yeyote chini ya Sheria Ndogo hii;-

a) kununua au kusafirisha mazao bila kibali cha Halmashauri,
b) kununua mazao shambani kabla hajavunwa,
c) kusafirisha mazao bila kulipa ushuru,
d) kununua mazao kwa kubadilishana na mali au nguo na kitu chochote kisichokuwa pesa,
e) kununua mazao nje ya eneo lililotengwa kwa ajili ya kuuza na kununulia mazao.

(8) Mnunuzi yeyote atawajibika kutoa taarifa sahihi ya mazao aliyonunua na kuonyesha risiti aliyolipia ushuru pamoja na kibali cha kununulia mazao kwa Afisa Mwidhiniwa mara atakapotakiwa kufanya hivyo.

(9) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukamata na kushikilia mazao yaliyonunuliwa kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii kwa muda wa siku saba (7).

(10) Endapo mmiliki hatakomboa mazao yake baada ya siku saba (7), Halmashauri itaomba kibali cha Mahakama ili kuuza mazao hayo kwa njia ya mnada

(11) Baada ya mnada, Halmashauri itakata fedha inazodai na gharama za kukamata, ulinzi na kuhifadhi mazao hayo na salio litakalobaki atapewa mmiliki wa mazao hayo.

Muda wa kusafirisha mazao

10. Itakuwa marufuku kwa mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 jioni hadi saa 12:00 asubuhi.

## SURA YA NANE
## USHURU WA MAEGESHO

Utengaji wa maeneo ya Maegesho

11 (1) Halmashauri itatenga maeneo kwa ajili ya maegesho ya magari madogo, magari makubwa pamoja na vyombo vingine vya usafiri.

Maeneo ya maegesho yatafunguliwa kuanzia saa

(2) 12:00 asubuhi na kufungwa saa 2:00 usiku.

(3) Halmashauri itaonyesha kwa alama au michoro ya maeneo ya maegesho kwa mistari au kwa namna yoyote ile itakayoashiria eneo la maegesho ya magari ili kuweka viwango vya kulipiwa.

(4) Kila chombo kitapaswa kuegeshwa maeneo maalum yaliyoainishwa na Halmashauri.

(5) Halmashauri inaweza kutoa kibali cha maegesho maalum kwa maombi maalum na malipo yake yatapangwa na Halmashauri kwa kipindi maalum.

(6) Mtu, Kampuni au Shirika ambalo litataka kuanzisha au kuwa na maeneo ya maegesho atapaswa kuomba kibali cha maegesho maalum na kutakiwa kulipia maegesho hayo kwa asilimia kumi (10%) ya mapato kadiriwa kwa mwezi na kupewa kibali husika.

(7) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho wa magari kwa magari yafuatayo;-

a) kwa magari yatakayoegeshwa stendi,
b) kwa magari yatakayoegeshwa nje ya stendi,
c) kwa magari yatakayoegeshwa maeneo mengine yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho katika eneo lolote ndani ya Mamlaka ya Halmashauri na si vinginevyo.

(8) Ushuru wa maegesho utalipwa na muegeshaji kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hii.

(9) Mtu yeyote atakayeegesha na kulipa ushuru wa maegesho kwa siku au kwa mwezi na kwa mkupuo ataruhusiwa kuegesha katika maeneo yoyote ndani ya Halmashauri pasipo kulipia tena ilimradi tu aonyeshe stakabadhi kutoka Halmashauri kuthibitisha uhalali wa malipo aliyolipa.

(10) Itakuwa marufuku kwa mtu yeyote;-

a) kutengeneza au kuosha gari ndani ya

maegesho

b) kuharibu miundombinu ndani ya maegesho

c) kutumia lugha ya matusi katika eneo la maegesho

(11) Ushuru wa maegesho utatozwa kwa magari yote kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii isipokuwa;-

a) magari ya Serikali,

b) magari ya kibalozi,

c) magari yaliyoegeshwa katika sehemu za ibada (muda wa ibada),

d) magari yaliyoegeshwa kwa ajili ya shughuli maalum za kitaifa na kwa muda huo tu.

(12) Halmashauri itakuwa na jukumu la kutoa vibali maalum kwa ajili ya maegesho maalum yatakayoombwa kupitia kwa Mkurugenzi.

## SURA YA TISA
## USHURU WA MINARA

Halmashauri kutoza ushuru wa Minara

12(1) Kutakuwa na tozo za minara yote iliyopo na itakayowekwa katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri.

(2) Ushuru wa minara utalipwa Halmashuri tarehe 01 Julai, mwanzoni mwa mwaka wa fedha husika kwa kiwango kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tisa la Sheria Ndogo hii.

## SURA YA KUMI
## ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI

Usajili wa vyombo vya usafiri

13(1) Kila chombo cha usafiri kinachofanya shughuli za biashara kitapaswa kusajiliwa Halmashauri kila mwaka.

(2) Kila chombo chenye usajili kitalazimika kulipiwa ada kama inavyoonekana katika Jedwali la Kumi Sheria Ndogo hii.

*Tangazo la Serikali Na. 275 (Linaendelea.)*

(3) Chombo cha usafiri kitakachosajiliwa kitapatiwa cheti cha usajili pamoja na stika iliyotayarishwa na Halmashauri. Stika hiyo itabandikwa sehemu inayoonekana katika chombo husika kama ushahidi wa malipo ya ada ya usajili.

(4) Ada ya usajili wa magari italipwa kabla ya tarehe 30 ya mwezi Juni ya kila mwaka. Baada ya tarehe hiyo mmiliki atalipa ada anayodaiwa pamoja na adhabu ya asilimia hamsini (50%) ya ada ya mwaka.

(5) Kila chombo kitapaswa kuegeshwa maeneo maalum yaliyoainishwa na Halmashauri.

SURA YA KUMI NA MOJA

Usajili wa maduka ya dawa na vituo binafsi vya kutolea huduma ya afya

(14)(1) Vituo vya afya, maduka ya dawa vinavyomilikiwa na watu binafsi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii zitatakiwa kusajiliwa.

(2) Mmiliki wa kituo binafsi cha kutolea huduma ya afya au duka la dawa atatakiwa kulipa ada ya usajili kama ilivyo ainishwa katika Jedwalila kwanza la Sheria Ndogo hii na ada ya usajili italipwa kabla ya huduma kutolewa.

SURA YA KUMI NA TATU

MAKOSA NA ADHABU

Halmashauri kuwajibika na mapungufu yake

(15) Halmashauri inaweza kuwajibishwa kwa kulipa hasara itakayosabishwa na Afisa Mwidhiniwa au Afisa yeyote ama kwa uzembe wake au kwa makusudi wakati wa kutekeleza majukumu yake yaliyokusudiwa na Sheria Ndogo hii kinyume au nje ya namna ilivyotakiwa.

Makosa

16(1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote chini ya Sheria Ndogo hii;-

a) kukataa au kukwepa kulipa ada na ushuru,
b) kushawishi mtu au kikundi cha watu kutolipa ushuru,
c) kumzuia au kujaribu kumzuia Afisa

Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii,

d) kujenga jengo lolote bila kibali cha ujenzi,
e) kuchinja mifugo bila kukaguliwa,
f) kufanya matangazo bila kuwa na kibali,
g) kuendesha gari kwa madhumuni ya biashara bila usajili,
h) kuegesha gari katika maeneo yasiyoruhusiwa

Adhabu

17 Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote viwili kwa pamoja faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

18 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Kumi na moja la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

*Tangazo la Serikali Na. 275 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 3(1))*

ADA YA VIBALI MBALIMBALI

| Na. | Aina ya Kibali | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kuweka uzio au fensi ya muda kwa ajili ya kufanya ujenzi ili kulinda usalama wa watu na mali. | Tshs 200/= kwa mita moja |
| 2. | Kibali cha mabadiliko ya matumizi ya ardhi. | Tshs. 100,000/= kwa ekari moja |
| 3. | Kibali cha kufanya matangazo ya biashara maeneo mengine nje na minada, masoko na magulio. | Kwa siku shilingi 50,000/= |
| 4. | Ada ya maombi ya usajili wa Vyombo vya usafiri. | Shilingi 2000/= kwa kila fomu ya maombi |
| 5. | Kibali cha mazishi (maeneo ya kuzikia yanayomilikiwa na Serikali) | Shilingi 10,000/= kwa kimoja |
| 6. | Kibali kwa ajili ya shughuli za kiutamaduni | Ngoma na shughuli nyingine za kiutamaduni- Tsh. 20,000/=kwa siku.<br><br>Matamasha na sherehe nyingine –Tsh 50,000/= kwa siku<br><br>Ada ya usajili waganga wa jadi au tiba mbadala – Tsh 50,000/= kwa mwaka. |
| 7 | Ada ya usajili wa vikundi vya kijamii (CBOs) | Tsh 30,000/= |
| 8 | Vikundi vingine ambavyo havijatajwa | Tsh 30,000/= |
| 9 | Meta 1 ya ujazo | Tshs 5,000/= kwa kwa kila meta I ya ujazo kwa tripu moja |
| 10 | Kuonyesha Mpira | Tshs. 2,000/= kwa siku |
| 11 | Pall table | Tshs 2,000/= kwa siku |
| 12 | Michezo ya kubahatisha | Tsh 50,000/= kwa mwezi |
| 13 | Fundi seremala | Tshs 30,000/= kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| 14 | Usajili wa duka la dawa | Tshs 100,000/= kwa mwaka |
| 15 | Usajili wa zahanati | Tshs 100,000/= kwa mwaka |
| 16 | Usajili wa kituo cha afya | Tshs 150,000/= kwa mwaka |
| 17 | Usajili wa Hospitali | Tshs 500,000/= kwa mwaka |
| 18 | Usajili wa duka la dawa muhimu | Tshs 50,000/= kwa mwaka |

ADA YA KUKODI MALI AU VIFAA VYA HALMASHAURI

| Na. | Aina ya Kifaa | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Ukumbi mkubwa wa Halmashauri | kuanzi shilingi 200,000/= kwa siku |
| 2. | Ukumbi mdogo wa Halmashauri. | Kuanzia shilingi 100,000/= kwa siku |
| 3. | Vyumba vya ofisi | Tsh 6,000/= kwa meta moja za mraba kiwango hiki kitabadilika kutokana na mkataba na baada ya kuridhiwa na baraza na madiwani. |
| 4. | Nyumba ya Utalii (Rest House) | Tsh.150,000/= kwa mwezi,kodi hii itabadilika kutokana na mkataba na baada ya kuridhiwa na baraza la madiwani. |
| 5. | Vibanda vya Biashara vilivyo jengwa katika maeneo ya Halmashauri katika kata ya Soni na Kwehengala. | Tshs. 50,000/= kwa mwezi |
| 6 | Kukodi viti vya Halmashauri | Tsh 500/= kwa kila kiti kwa siku |

JEDWALI LA PILI

Limetungwa chini ya kifungu cha 4 (1)

ADA YA UPIMAJI AFYA NA UKAGUZI WA AFYA.

| Na. | Aina ya Ada | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Upimaji afya | Shilingi 6,000/= Kila baada ya miezi sita |
| 2 | Ada ya ukaguzi, nyumba za starehe, Baa na Vilabu vya pombe | Tsh 10,000/= Kila baada ya miezi sita |

| | | |
|---|---|---|
| | za kienyeji | |
| 3 | Nyumba za kulala wageni | Tsh 10,000/= kila baada ya miezi sita |
| 4 | Maduka ya bidhaa | Tsh 10,000/= Kila baada ya miezi sita |
| 5 | Nyumba za kutengeneza na kuuzia vyakula na nyama choma | Tsh 10,000/= Kila baada ya miezi sita |
| 6 | Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara | Tsh 10,000/ = Kila mwaka |
| 7 | Ukaguzi wa viwanda vikubwa | Tsh 100,000/= Kila baada ya miezi sita |
| 8 | Ukaguzi wa viwanda vya kati na karakana | Tsh 50,000/= Kila baada ya miezi sita |
| 9 | Ukaguzi wa viwanda vidogo | Tsh 20,000/= Kila baad ya miezi sita |
| 10 | Mama ntilie, Baba lishe na magenge ya aina zote | Tsh 5,000/= Kila baada ya miezi sita |
| 11 | Masuala ambayo hayajatajwa na yanahitaji ukaguzi | Tsh 5,000/= kila baada ya miezi sita |

JEDWALI LA TATU

Limetungwa chini ya kifungu cha 5(2)

A: VIBALI VYA UJENZI

| Na. | Aina ya Ada | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Meta moja ya ujazo | Tsh 500 kwa kila meta moja ya Mraba |
| 2. | Ada ya maombi ya kibali cha ujenzi (Fomu) | Tshs. 20,000 kwa kila fomu |

B: KIBALI CHA KUJENGA UZIO WA KUDUMU

| Na. | Ukubwa wa eneo | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | Meta moja ya ujazo | Tsh.500 kwa kila meta moja ya Mraba |

C: KIBALI CHA KUJENGA MINARA (INSTALLATION CHARGES)

| Na. | Idadi | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | Kila mnara mmoja | Ths. 1,000,000/= |

JEDWALI LA NNE

Limetungwa Chini ya kifungu Cha 6(1)

ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

| Na. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Tozo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 3000/= | Kwa kila Ng'ombe |
| 2. | Mbuzi au Kondoo | 2000/= | Kwa kila Mbuzi au Kondoo |
| 3. | Mnyama mwingine yeyote | 2000/= | Kwa kila atakayechinjwa |
| 4. | Nguruwe | 2000/= | Kwa kila atakayechinjwa |
| 5 | Ushuru wa ngozi ya ng'ombe | 200/= | Kwa kila kipande cha ngozi |
| 6 | Ushuru wa ngozi ya Mbuzi au Kondoo | 100 | Kwa kila kipande cha ngozi |

JEDWALI LA TANO

Limetungwa chini ya kifungu cha 7

USHURU WA SOKO LA WANYAMA NA NDEGE

| Na. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Tozo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe, Ngamia, Punda na Farasi | 4000/= | Kwa kila Ng'ombe au Punda kwa siku |
| 2. | Mbuzi, Kondoo na Nguruwe | 1000/= | Kwa kila Mbuzi au Kondoo kwa siku |
| 3. | Mnyama mwingine yeyote | 1500/= | Kwa kila mnyama kwa siku |
| 4. | Kuku, bata na wengine wanaofanana na hao | 200/= | Kwa kila ndege kwa siku |

JEDWALI LA SITA

Limetungwa chini ya kifungu cha 8 (1)

KODI, USHURU NA ADA KWA MATUMIZI YA MASOKO NA MAGULIO NA MAENEO MENGINE

| Na. | Aina ya biashara | Kiwango cha Tozo | Idadi |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Kodi ya pango ya chumba au fremu | 20,000/= | Kwa chumba kimoja kwa mwezi kodi hii itakuwa inabadilika kutokana na bei ya soko na baada ya kuridhiwa na Baraza la Madiwani. |
| 2. | Ushuru wa soko, magulio na minada | 500/= | Kwa siku |
| 3. | Ushuru wa kuuza chakula mama lishe na baba lishe | 2000/= | Kwa siku |
| 4. | Ushuru wa tenga la nyanya, hoho, pilipili, bilinganya, bamia, nyanya chungu, karoti, matunda na vingine vinavyofanana na hivyo. | 500/= | Kwa kila tenga |
| 5. | Ushuru wa mkungu wa ndizi | 300/= | Kwa kila mkungu |
| 6. | Ushuru wa magunia ya nafaka yanayoshushwa ndani ya soko kama mahindi, mchele, kunde, choroko, maharage, mbaazi na mazao mengine nje ya nafaka. | Asilimia tatu (3%) ya bei ya mazao husika kwa bei ya shamba | Kwa kila gunia lenye ujazo wa kilo mia moja. |
| 7. | Ushuru wa kufanya matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti katika masoko, magulio na minada | 10,000/= | Kwa siku |
| 8. | Ushuru wa vizimba | 15,000/= | Kwa mwezi |
| 9. | Ushuru wa choo | Haja ndogo na kubwa - 300<br><br>Huduma ya kuoga - 500 | Kwa kila inapohitajika huduma |
| 10. | Ushuru wa meza ndani ya soko | 1000/= | Kwa kila siku ya soko |
| 11. | Ushuru wa vyombo vya usafiri vitakavyoingia katika Magulio, Masoko na Minada ya Halmashauri | Gari la zaidi ya Abiria 39<br><br>Gari la Abiria 20 – 39<br><br>Gari dogo la abiria chini ya abiria 20<br><br>Teksi<br><br>Magari binafsi | Tshs 2000/= kwa siku<br><br>Tshs. 1500/= kwa siku<br><br>Tshs. 1000/= kwa siku |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Gari dogo la mizigo chini ya tani 7<br><br>Gari kubwa zaidi ya tani 7<br><br>Pikipiki (Bodaboda)<br><br>Mikokoteni ya aina zote | Tshs. 2000/= kwa siku<br><br>Tshs. 200/= kwa siku<br><br>Tshs. 2000/= kwa siku<br><br>Tshs. 2500/= kwa siku<br><br>Tshs. 500/= kwa siku<br><br>Tshs. 500/= kwa siku |
| 12. | Ada ya kupata kibali cha kufanya biashara ya mazao ya misitu | Mkaa<br><br>Mbao<br><br>Kuni<br><br>Nguzo<br><br>Fito<br><br>Kibali cha kukata au kuvuna mti wa kupandwa<br><br>Kibali cha kukata au kuvuna mti wa asili | Tshs. 200,000/= kwa mwaka<br><br>Tshs. 200,000/= kwa mwaka<br><br>Tshs 100,000/= kwa mwaka<br><br>Tshs 100,000/= kwa mwaka<br><br>Tshs 100,000/= kwa mwaka<br><br>Tshs 20,000/= kwa mwaka<br><br>Tshs 2,000/= kwa mti mmoja<br><br>Tshs 10,000/= kwa mti mmoja |
| 13 | Kukodi vitivo au shamba vinavyo milikiwa na Halmashauri | Kitivo<br><br>Shamba ambalo sio kitivo | Tshs. 260,000/= kwa ekari 1 kwa mwaka<br><br>Tshs. 50,000/= kwa msimu 1 wa kilimo. Kodi hizi zitakuwa zikibadilika kutokana na gharama halisi kwa wakati huo na baada ya kuridhiwa na Baraza la Madiwani. |

JEDWALI LA SABA

Limetungwa chini ya kifungu cha 9(2)

USHURU WA MAZAO

*Tangazo la Serikali Na. 275 (Linaendelea.)*

| Na. | Aina ya mazao | Kiwango cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Mazao ya biashara | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 2. | Mazao ya chakula | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 3. | Mazao ya misitu | 5% ya bei ya kununulia shambani |

JEDWALI LA NANE
Limetungwa chini ya kifungu cha 11(7)
USHURU WA MAEGESHO

| Na. | Muda wa uegeshaji | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Nusu saa | Shilingi 300/= |
| 2. | Saa moja | Shilingi 600/= |
| 3. | Siku nzima | Shilingi 1,000/= |
| 4. | Kulaza gari kwenye maeneo yanayomilikiwa na halmashauri | Shilingi 5,000/= kwa usiku mmoja |

JEDWALI LA TISA
Limetungwa chini ya kifungu cha 12(2)
USHURU WA MINARA

| Na. | Idadi ya minara | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Kila mnara mmoja | Usiopungua shilingi 1,000,000/= kwa mwaka |

JEDWALI LA KUMI
Limetungwa chini ya kifungu cha 13(1)
ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI

| Na. | Aina ya chombo | Kiwango cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Taxi/kirikuu | 30,000/= kwa mwaka |
| 2. | Gari chini ya tani 7 | 40,000/= kwa mwaka |
| 3. | Gari zaidi ya tani 7 | 50,000/= kwa mwaka |
| 4. | Bajaji/ toyo ( pikipiki matairi mitatu ) | 30,000/= kwa mwaka |
| 5. | Pikipiki ( tairi mbili ) | 20,000/= kwa mwaka |

JEDWALI LA KUMI NA MOJA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 18)*

HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi...............................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ............................................................ ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli kwamba tarehe ..................... ya mwezi ....................... mwaka ........................... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .............................. cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli ya mwaka 2021.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, nipo tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe.....................ya mwezi.........................mwaka.....................................

Jina.................................................... Saini...........................................................

Mbele ya:

Jina:................................................Cheo:............................................

Saini.....................................................................................................

Nembo ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa baraza la Madiwani la Halmashari ya Wilaya ya Bumbuli uliyofanyika mnamo tarehe 19/2/2020 na Nembo iliyogongwa mbele ya:-

GEORGE D. HAULE,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*BUMBULI*

Amiri A. Sheiza,
Mwenyekiti,
*Halmashauri ya Wilaya,*
*BUMBULI*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Novemba, 2021

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi*